

BODI YA USAJILI WA MAKANDARASI (CRB)



MIKUTANO YA MASHAURIANO NA WADAU WA SEKTA YA UJENZI KWA MWAKA 2021

“Juhudi za Makusudi za Wadau Kuwezesha Ukuaji wa Makandarasi wa ndani”.

Mbeya; Tarehe 22 - 23 Aprili 2021, Ukumbi wa Tughimbe

Arusha; Tarehe 6 - 7 Mei 2021, Ukumbi wa Corridor Springs

Dar es Salaam; Tarehe 27 - 28 Mei 2021, Ukumbi wa Diamond Jubilee

Mwanza; Tarehe 10 - 11 Juni 2021, Ukumbi wa Gold Crest

Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) inapenda kuwataarifu **Makandarasi** na wadau wote wa Sekta ya Ujenzi wakiwemo **Waajiri, Wataalam Washauri** (Wahandisi, Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi) na wataalam mbalimbali katika sekta ya ujenzi kuwa imeandaa mikutano ya kikanda ya mashauriano na wadau wa sekta ya ujenzi katika mikoa ya, **Mbeya (Tarehe 22 - 23 Aprili 2021, Ukumbi wa Tughimbe), Arusha (Tarehe 6 - 7 Mei 2021, Ukumbi wa Corridor Springs), Dar es Salaam (Tarehe 27 - 28 Mei 2021, Ukumbi wa Diamond Jubilee) na Mwanza (Tarehe 10 - 11 Juni 2021, Ukumbi wa Gold Crest).** Katika vituo vyote, mikutano itanza saa 2.00 asubuhi. Kaulimbiu ya mikutano ni: *“Juhudi za Makusudi za Wadau Kuwezesha Ukuaji wa Makandarasi wa ndani”;* na mada zifuatazo zitajadiliwa:-

- Uzoefu wa CRB kuhusu changamoto zinazoathiri ukuaji wa makandarasi nchini
- Mtazamo wa Makandarasi kuhusu changamoto zinazoathiri ukuaji wao
- Tathmini ya Utekelezaji wa vifungu wezeshi vya sheria ya manunuzi ya umma kwa ukuaji wa makandarasi
- Mtazamo wa Waajiri kuhusu changamoto zinazoathiri ukuaji wa makandarasi
- Uzoefu wa wataalam washauri kuhusu changamoto zinazoathiri ukuaji wa makandarasi
- Uzoefu wa Makandarasi wa kigeni kuhusu changamoto zinazowakabili makandarasi wa ndani

Katika kituo cha Dar es Salaam, mkutano pia utaambatana na maonesho ya Teknolojia, huduma na vifaa vya ujenzi.

Walengwa	Makandarasi, Wataalam washauri; Wabunifu Majengo, Wakadiriaji Majenzi, Wahandisi, Wataalam wanaoashabihiana nao, Waajiri, Watunga sera za uwezesaji wananchi kiuchumi, watumishi wa taasisi za Serikali zenye dhamana ya manunuzi ya umma katika shughuli za ujenzi na wadau wote wa Sekta ya Ujenzi wanaalikwa kushiriki.
Ada ya Ushiriki	Ada ya ushiriki ni TZS 50,000/= kwa Makandarasi na TZS 100,000/= kwa Wadau wengine. Ada itagharamia mahitaji ya mkutano kama ukumbi, chakula cha mchana na vinywaji. Ada ya ushiriki italipwa kwa utaratibu ufuatao:- Malipo ya ada ya ushiriki yafanywe benki ya CRDB Plc au NBC Ltd. , au NMB Plc kwa jina la CONTRACTORS REGISTRATION BOARD pia kwa kupitia mitandao ya simu kwa kutumia “Control Numbers katika vituo husika” kama ifuatavyo:- Makandarasi Mbeya: “Control Number” 995740029796 Arusha: “Control Number” 995740029798 Dar es Salaam: “Control Number” 995740029791 Mwanza: “Control Number” 995740029794

Wadau wengine

Mbeya: "Control Number" **995740029797**

Arusha: "Control Number" **995740029799**

Dar es Salaam: "Control Number" **995740029792**

Mwanza: "Control Number" **995740029795**

Hakikisha **namba ya simu ya mshiriki** imeoneshwa katika karatasi ya malipo ya benki.

**Maonesho
(Exhibitions)**

Bodi inayaalika makampuni na watu binafsi kushiriki kwa kuonesha teknolojia, huduma, bidhaa, vifaa na zana za Ujenzi kwa lengo la kuzitangaza kwa wadau wa sekta ya ujenzi **katika mkutano wa kituo cha Dar es Salaam**. Watakaopenda kushiriki maonesho hayo wawasiliane na **Ndugu Alois Manamba** kwa simu namba **0715809473** au kwa barua pepe kwa anwani almanamba@gmail.com au crbhq@crbtz.org

**Jinsi ya
Kujisajili**

Washiriki wathibitisha kuhudhuria mkutano kwa kulipa ada ya ushiriki angalau siku kumi (10) kabla ya tarehe ya mkutano katika kituo husika na kutuma majina na mawasiliano yao katika ofisi yoyote ya **CRB** nchini. **Washiriki wanahimizwa kujisajili mapema ili kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza.**

**Mafunzo
endelevu
(PDU)**

Washiriki ambao ni wataalam kama Wabunifu majengo, Wakadiriaji majenzi na Wahandisi watakaoshiriki mkutano huu watatuzwa alama **16** za mafunzo endelevu zitatolewa zitakapombwa katika Bodi zao za usajili.

Kwa taarifa zaidi fanya mawasiliano kama ifuatavyo:-

CRB Makao makuu, S.L.P 13374 Dar es Salaam Simu 022 213 1169, Tovuti: www.crb.go.tz, Barua pepe: crbhq@crbtz.org

CRB Kanda ya Mashariki, S.L.P 33621 Dar es Salaam Simu 022 2771877, Barua pepe: crbez@crbtz.org

CRB Kanda ya Ziwa, S.L.P 2815 Mwanza Simu 028 2500218, Barua pepe: crblz@crbtz.org

CRB Kanda ya Kusini, S.L.P 1690 Mbeya Simu 025 2502480, Barua pepe: crbsz@crbtz.org

CRB Kanda ya Kaskazini, S.L.P 16795 Arusha Simu 027 2547107, Barua pepe: crbnz@crbtz.org

CRB Kanda ya Kati, S.L.P 2618 Simu 026 2966040, Barua pepe: crbcz@crbtz.org